



## UKWELI JUU YA UBATIZO WA MAJI

(The Truth about Water Baptism)

UTANGULIZI:

Yesu, Mungu allye dhíhíríshwa litatíka mwili, alisema, "Mkinipenda mtazishika amri zangu" (Yohana 14:15). Yesu huyu anatvdambia ya kwamba, "Yule atakaye weka imaní yake kwangu na kubatizwa ataokoka kutohana na adhabu ya dhambi" (Marko 16:16) Ukipenda Yesu, basi utatenda jinel anavyo kuamuru ubatízwe litatíka Jlna la Yesu. Wale° hawaamini mambo haya, baasí adhabu inawangojea.

Unapo tubu dhambi zako na kumuulíza Mungu akusamehe, basi iinakufia dhambi zako. Baada ya mtu kufia, huzikwa. Baada ya mtu kufia dhambi zake inahitaji azikwe katika ubatizo (Warurni 6:4). Unapo mtii Mungu katika Ubatizo kwa Jina la Yesu, dhambi zako za kale zinapata kuoshwa, naye Mungu anakusamehe.

JE, NIBATIZWE NAMNA GANI?

Mwanadamu ametengeneza njia tofauti za kubatiza. Wengine hunyunyizia maji, wengine hum- wagiHa maji, wakati weringine wanapo kuzamisha kwenye maji. Waefeso 4:5, yatuwambia, "Kunaye Bwaria Mmoja, imani moja na Ubatizo mmoja." Je, ni njia gani

mojawapo hizi illyo sawasawa? Jinsi Biblia Ilivyo Maandishi ya Mungu ya Kweli, basi aina ya Ubatizo uliyo tumiwa katika Biblia ndiyo wa kweL Njia aliyo batizwa Yesu, ndiyo njia ya pekee iliyo ya kweli.

#### UBATIZO UNAENDELEA:

Biblia inasema, "Yesu aHpanda kutoka majini" (Mathayo 3:16). Nerio la Mungu pia linatwambia kwamba tunazikwa wakati tunapo batázwa. Hauwezl kunyunyuzia mtu mchanga kidogo tij anapo zikwa baada ya kufa. Hivyo hivyo, hautakiwi kuwa nyunyiziwa maji kidogo wakato unapo batizwa. Nerio Ubatizo kwa kweli lilitokana nalo neno la Kiyunani"batizo" ambalo maana yake ñí kutumbukiza, au kuzamisha.

Kuweza Icubatizwa kwa njla iliyo sawasawa, unahitaji kufunikwa kabisa kwenye maj.

Sio kwamba watu wanazo tu njia tofauti za ubatizo, lakini pia wanayo maneno ambayo hao husema wanapo batiza. Kama jinsi tunavyo fahamu kwamba kunao UBATIZO MMOJA, basi tunafahamu kwamba ni lazima kusema maneno yallyo tumika katika Biblia wakati watu wote walipo batizwa.

Baada ya kanisa kuanza katíka fflatendo ya Mitume 2, hatuna habari yo yote juu ya mtu aliye batizwa maneno mengine yaktumiwa isipokuwa "Katika Jina la Yesu Kristo."

Siku ya Pentekoste, habari zilizo katika Matendo ya Mitume 2, wakati kanisa lilianza, Petro ndiye allye kuwa Mhubiri kwa mitume. Yesu alikuwa amempa " funguo za Ufalrne wa Binguni" (Mathayo 16:19). Basi watu walipo muuliza Petro jinsi ya kuweza kuokoka, aHki.iwa nayo mamlaka kutoka kwa Mungu kuwaambia. "Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila rñoja wenu katika Jina la Yesu Kristo nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu (Matendo ya Mitume 2:38). Watu elfu tatu walitii maneno haya ya Wokovu slku hiyo na wakabatizwa.

#### UBATIZO UNAENDELEA:

Filipo aliwabatiza Wasamaria katika Matendo ya Mitume 8 katika Jina la Yesu. Paiilo aliliitia Jina la Yesu Icatika Ubatizo wake.Petro alirnbatiza Kornelio na jamaa wake, katika Jina la Yesu

kwenye Matendo 10. Paulo akawabatizwa watu tena katika Ulatendo ya Mitume 19 baada tu ya kutambua kwamba walikuwa bado havwaja batizwa katika Jina la Yesu.

"Nakila mfanyalo, kwa neno au kwa tendu, fanyeni yote katika Jina la Bwana Yesu." (Wakolosal 3:17). Hakuna njia yo yote ya kuweza kuepukana nayo adhabu ya dhambi kuitia awaye ye yote. Kwamaana hakuna Jina lingine chini ya mbingu lililo pewa mwanadamu limpasalo kuokolewa kwalo" (Matendo ya Mitume 4:12). Maandishi haya mawili yanatia mkazo umuhimu vya kutumia jina la Yesu katika Ubatizo.

#### KUMALIZA:

Mungu katika Neno lake, Biblia, ameamuru kwvamba ubatizvwe. Amekufanya ufahamu kwamba Icunayo njia moja tu iliyo sawa kubatizwa, nayo njia hii ni, kuzamishwa kwenye maji katika Jina la Yesu.

Katika Yohana 14:15, Yesu anasema, "Mkinipenda mimi, mtashika amri zangu. Usipo til ne kubatizwa, basi haumpendi, na karna haumpendi basi hauwezi kuolcoka tokane na adhabu ya dhambi zako. Walakini, kwa kuunyesha upendo wako kwa Mungu katika kutubu na kubatizwa katiks Jina la Yesu, dhambi zako zitasamehewa na utapokea kipawe che Roho fItakatifu. (Matendo 2:38)

Neno la Mungu linasema kwako kama jinsi Anania alimwambia Paulo, "Unakewilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia Jina Lake. (Matendo 22:16)